HOTUBA YA MKUU WA WILAYA YA RUFIJI MHESHIMIWA JUMA NJWAYO KATIKA MAADHIMISHO YA KILELE CHA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA TAREHE 16 JUNI 2017, INAYOFANYIKA KI-WILAYA KATIKA KATA YA UTETE, WILAYA YA RUFIJI.

Wah: Madiwani Kata ya Utete na Chemchem,
Ndg: Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji,

Ndg:Wakuu wa Idara,

Ndg: Viongozi wa Kata,

Ndg: Waalikwa wote,

Ndg: Wananchi,

Watoto, Mabibi na Mabwana.

Asalaam Alleykhum.

Bwana Yesu Asifiwe.

Awali ya yote nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza waandaaji wa maadhimisho haya, pia niwashukuru kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi. Aidha, niwashukuru na kuwapongeza Viongozi na Wananchi wa Kata ya Utete Wilaya ya Rufiji kwa kukubali jukumu la kuwa wenyeji wa siku hii ya mtoto wa Afrika Ki-Wilaya. Ahsanteni sana.

Ndugu Wananchi,

Maadhimisho haya hufanyika tarehe 16 June ya kila mwaka. Siku hii inaadhimishwa kufuatia kupitishwa kwa Azimio la nchi 51 wanachama wa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika(OAU) kwa ajili ya kukumbuka mauaji ya kinyama waliyofanyiwa watoto wa kitongoji cha Soweto nchini Afrika ya kusini mwaka 1976. Kwa sasa Siku hii inasaidia kuangalia mafanikio yaliyopatikana, changamoto tunazokabiliana nazo katika malezi ya watoto na kuona juhudi mbali mbali zinazofanywa na serikali katika kumwendeleza mtoto, kuhamasisha jamii kuhusu utekelezaji wa sera, mipango na program mbalimbali za kumuendeleza mtoto.

Ndugu Wananchi,

Kauli mbiu ya mwaka huu inasema **"Maendeleo endelevu 2030:Imarisha Ulinzi na Fursa Sawa kwa Watoto"** lengo la kauli mbiu hii ni kusisitiza na kuwakumbusha wadau na jamii kwa ujumla kushiriki kiamilifu katika utekelezaji wa agenda ya 2030 ya maendeleo endelevu juu ya ulinzi na fursa sawa kwa mtoto. Tunapozungumzia suala la ulinzi kwa mtoto inahusisha kuwakinga dhidi ya adhabu kali, ubakaji, ulawiti, unyanyasaji na mimba za utotoni.
Aidha fursa sawa ni pamoja na kuhakikisha kuwa watoto wote wa kike na wakiume wanapata fursa sawa ya elimu, afya na kupewa nafasi ya kutoa maoni katika ngazi ya familia na jamii kwa ujumla.

Ndugu wananchi
Wilaya yetu imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali katika suala zima la ustawi wa mtoto ikiwa ni pamoja na mimba katika umri mdogo, utoro shuleni na adhabu kali, hali inayopelekea kudumaza maendeleo ya watoto kielimu na kiafya, hivyo ni jukumu la kila mzazi na jamii kuhakikisha kuwa watoto wanapata haki zao za msingi ikiwa ni pamoja na kulindwa, kusikilizwa,kuishi, kupatiwa matibabu na elimu.
Tukumbuke kuwa elimu ndio msingi wa maendeleo hivyo ni jukumu letu kuhakikisha watoto wanahudhuria shuleni na kujua maendeleo yao pia kuongeza ushirikianao baina ya wazazi na waalimu, kwakufanya hivyo tutaongeza ubora wa elimu kwa watoto. Nachukua fursa hii kuwaagiza wananchi wote Wilaya ya Rufiji kusimamia kikamilifu sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kufanyiwa marekebisho ya mwaka 2002 inayozungumzia masuala ya uandikishaji wa wanafunzi, ufundishaji, adhabu, utoro n.k. Aidha, wahusika wote wanaosimamia sheria hiyo waendelee kuwajibika ipasavyo kuisimamia sheria hiyo ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo.

TAKWIMU ZINAZOONYESHA VITENDO VYA KIKATILI DHIDI YA WATOTO WILAYA YA RUFIJI KWA KIPINDI CHA JULAI 2016 HADI JUNI 2017.

Jumla ya makosa yaliyoripotiwa ni 170 kama ifuatavyo;

NAMBA	AINA YA KOSA	IDADI
1	UBAKAJI	50
2	KUNAJISI	05
3	MIMBA	25
4	KUJERUHI	15
5	SHAMBULIO	65
6	KULAWITI	10
	JUMLA YA MAKOSA	**170**

Chanzo cha takwimu ni Ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya

TAKWIMU ZA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI WALIOACHA SHULE KWA SABABU YA UTORO NA MIMBA WILAYA YA RUFIJI KWA KIPINDI CHA JANUARI 2017 HADI JUNI 2017.

NAMBA	SABABU ZA KUACHA SHULE	WAV	WAS	JUMLA
1	UTORO	260	121	381
2	MIMBA		03	03

Chanzo cha takwimu ni Idara ya Elimu Msingi Wilaya

TAKWIMU ZA WANAFUNZI WATORO, WAJAWAZITO NA WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU KWA KIPINDI CHA JULAI 2016 HADI JUNI 2017

NA	JINA LA SHULE	UTORO		MIMBA	MAZINGIRA MAGUMU	
		WAV	WAS	WAS	WAV	WAS
1	MBWARA SEKONDARI	0	0	02	0	0
2	UTETE SEKONDARI	02	0	0	0	0
3	UMWE SEKONDARI	02	03	0	76	76
4	IKWIRIRI SEKONDARI	0	0	0	68	48
5	MOHORO SEKONDARI	20	06	05	96	63
6	NGORONGORO SEKONDARI	11	05	0	70	72
7	MWASENI SEKONDARI	03	0	01	88	68
8	KAZAMOYO SEKONDARI	0	08	04	84	116
9	MKONGO SEKONDARI	23	09	02	27	09
	JUMLA KUU	**61**	**31**	**14**	**509**	**452**

Chanzo cha takwimu ni Idara ya Elimu Sekondari Wilaya

Ndugu Wananchi,

Nasisitiza umuhimu wa kutunza familia zetu, wazazi lazima wawe mstari wa mbele katika kuhakikisha mtoto anapata haki zake za msingi ikiwa ni pamoja na haki ya kusikilizwa, kulindwa, kuheshimiwa na kupata huduma bora za malazi, mavazi na chakula. Aidha, Unyanyasaji wa watoto bado ni tatizo katika jamii yetu. Unyanyasaji huu upo katika vitendo vya ubakaji,ulawiti, ukatili wa vipigo na kufanyishwa kazi ngumu. Natoa wito kwa wazazi wote Wilaya ya Rufiji, tuwajibike kuhakikisha vitendo vya kikatili dhidi ya watoto vinatokomezwa. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wale wote watakao bainika kuwa wanatenda vitendo vya kikatili kwa watoto.

Ndugu Wananchi,

Pamoja na changamoto zinazowakabili watoto, yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta ya Afya na Elimu katika Wilaya yetu ikiwa ni pamoja

na wazazi na walezi kujitokeza kuwaandikisha watoto kujiunga na masomo ya shule za msingi na sekondari. Aidha wazazi wameitikia wito wa kuwapeleka watoto katika Kliniki ya baba, mama na mtoto ili wapate huduma za afya ikiwa ni pamoja na chanjo.

Zifuatazo ni takwimu zinazoonyesha uandikishaji wa watoto katika shule za msingi na sekondari.

TAKWIMU ZA UANDIKISHAJI WANAFUNZI WA DARASA LA AWALI KATIKA SHULE ZA MSINGI WILAYANI RUFIJI JANUARI 2017

MALENGO YA UANDIKISHAJI			UANDIKISHAJI HALISI			
WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA	%
1512	1486	2998	1336	1302	2638	88

Chanzo cha takwimu ni Idara ya Elimu Msingi Wilaya

TAKWIMU ZA UANDIISHAJI WANAFUNZI WA DARASA LA KWANZA KATIKA SHULE ZA MSINGI WILAYA YA RUFIJI JANUARI 2017.

MALENGO YA UANDIKISHAJI			UANDIKISHAJI HALISI			%
WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA	
2479	2295	4775	2706	2493	5199	109

Chanzo cha takwimu ni Idara ya Elimu Msingi Wilaya

TAKWIMU ZA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA JANUARI 2017

WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA	WANAFUNZI WALIORIPOTI	%

KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA			SHULENI			
WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA	
532	543	1079	517	530	1047	97

Chanzo cha takwimu ni Idara ya Elimu Sekondari Wilaya

TAKWIMU KUTOKA KLINIKI YA BABA MAMA NA MTOTO

	JANUARI-DISEMBA 2016			JANUARI-MEI 2017		
WAALIOMALIZA CHANJO	WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA
	1364	1448	2812	694	689	1383
UZITO MZURI	29867	30369	60236	13726	13414	27140
UZITO DHAIFU	6415	6712	13127	1571	1784	3355
UZITO DHAIFU SANA	531	392	923	82	101	183

Chanzo cha takwimu ni Idara ya Afya Wilaya

Ndugu Wananchi,

Mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kufanikisha maadhimisho haya, nawapongeza wananchi wote mliojitokeza kwa ajili ya siku hii muhimu ya mtoto wa Afrika.

Asanteni sana kwa kunisikiliza